KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 15, Issue 4

30th Dhul Qa'dah 1432

28th Oct, 2011

YALIYOMO

HAJJ NA MAHRAM 1 - 4

SWALA UKIWA JELA 2 - 3

WAKE ZAKE MTUME WALIKWENDA HAJJ BILA YA MAHRAM ?

Na: Sheikh Saalih al-Munajjid

Suali: Wake za Mtume (صلى الله عليه وسلم) walihijji mara nyingi baada ya kufa Kwake. Je, hii ni dalili yakuwa mwanamke aweza kuhijji bila ya mahram akiwa na wanawake wenzao wenye mahram?

Jawabu: AlhamduliLlaah hoja iliyo ya sawa ni hoja ya wanavyuoni wa ki-Hanafi na Hanbali, ambao wasema haifai kwa wanawake kusafiri kwenda hajj au safari nyengine bila ya Mahram, kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: "Hakuna mwanamke kusafiri bila ya mahram" [al-Bukhari &Muslim]. Lakini baadhi ya wanavyooni wa ki-Shafii na Maalik, na baadhi ya Salaf, walikuwa na maoni yakuwa mwanamke aruhusiwa kwenda Hajj bila ya Mahram akiwa atakuwa na kundi lenye uaminifu. Wananukulu kama ushahidi uanotajwa na muulizaji, kuwa wake za Mtume (صلى الله عليه وسلم) walifanya hajj bila ya mahram. Inasemekana kuwa Umar ibn al-Khattab (رضي الله عنه) aliwapa ruhusa wakeze Mtume (صلى الله عليه وسلم) kufanya hajj aliyoifanya yeye ya mwisho, akawatuma kuandamana nao Uthmaan ibn 'Afaan na Abd al-Rahman ibn 'Awf (رضي الله عنهم) pamoja nao.

Wanavyuoni wenye kushikilia hoja ya kwanza wametaja baadhi ya mambo kama ushahidi wao, nayo ni kama ifuatavyo:

1- Wamesema haikutajwa katika hadeeth kuwa hawakuwa na mahram. Labda mahram zao walikuwa pamoja nao kwenye msafara huo huo. Na 'Umar ibn al-Khattab (رضي الله عنه) aliwatuma Uthmaan ibn Affaan na Abdurahmaan ibn Awf (رضي الله عنهم) kama alama ya heshima ya nyongeza kwa Ummu al-Muumineen (رضي الله عنها) na wawe na Utulivu na Salama kwenye safari hiyo. Haiwezi kudhaniwa kuwa Maswahaba (رضي الله عنهم) watakwenda kinyume cha maamrisho ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuwa wanawake wasisafiri bila ya mahram, hasa kuwa baadhi ya riwaya ingawa sanad zake zina utata zaonyesha kuwa mahram zao walikuwa wapo.

Ibn al-Jawzi kwenye *al-Muntadham*, kuhusu matukio ya 23 al-hijra, alisema kuwa Abu 'Uthmaan, Abu Haarithah na al-Rabee walisema kuwa "Umar (رضي الله عنه) alifanya Hajj pamoja na wakeze Mtume (صلى الله عليه وسلم) ambao walikuwa na mahram zao ambao hawana lazima ya kutekeleza hijab. Mbele ya msafara alimtanguliza Abdulrahmaan ibn Awf (رضي الله عنه) na nyuma Uthmaan ibn Affaan (رضي الله عنه). Na ni aghlabu kuwa mahram zao hawakuwepo, kwa sababu watu wengi huwenda Hajj pamoja nao kutoka Madeenah. Yawezekana mno kuwa ndugu, ma-babu, ma-khale, ma-Ammi, au mahram zao kwa kunyonya, kwa sababu kunyonyesha watoto wa wengine ni jambo la kawaida zama zile.

2- Ikiwa tutachukulia yakuwa mahram zao hawakuwepo, basi huweda ikawa ni ijtihaad zao. Na ni maalum kuwa ijtihaad ya Maswahaba haikubaliwi ikiwa itapingana na hadeeth swaheeh ya Mtume (صلى الله عليه وسلم). As-San'aani (رحمه الله) alisema: "Hilo haliwezi kuchukuliwa kama ushahidi kwa kuwa hakuna ijmaa'. (*Subul al-Salaam* 2/930)

3- Kundi la tatu la ma-'Ulamaa walijadili wakasema kuwa jambo hili liliwahusu wakeze Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa sababu wao ni mamama wa waumini na wanaume wote ni mahram zao.

Abu Haneefah (رحمه الله) alisema: "Watu wote walikuwa ni mahram kwa Aaisha (رضي الله عنها), kwahivyo haijalishi kwa yoyote kusafiri nae bali ni mahrim yake, na hilo haliwahusu wanawake wengine ila wake za Mtume (صلى الله عليه وسلم) (*Umdat al-Qaari* -10/220)

Lakini jibu hili la Abu Haneefah (رحمه الله) halikubaliki, kwa sababu wakeze Mtume (صلى الله عليه وسلم) walikuwa ni mahram zao na mama wa waumini kuhusu wao hawawezi kuolewa nao, ama kuhusu mengine si mahram. Ikiwa waumini ni mahrim ingekuwa waruhusiwa kuvua hijabu mbele zao, kuwa peke nao na mengine na hakuna awezae kujasiri kuyadhania hayo.

Ibn Taymiyah (رحمه الله) amesema kuhusu wake za Mtume (صلى الله عليه وسلم) wao ni mama za waumini yakuwa wao waumini, ni haramu kwao, yoyote kuwaoa, sio kuwa ni mahram kwa mengine (*Manhaaj al-Sunnah*-4/207). Jibu la kwanza ndilo bora.

Kumalizia: Hairuhusiwi kukataa hadeeth swaheeh kwa sababu ya ufahamu wa baadhi ya vitendo vya Maswahaba ambao ina ufaumu zaidi ya mmoja. Ninalotakiwa nikulifuata lile lililothubutu na wala si kufuata yanayoingia katika tafsiri nyingi.

Shykh Abd al-Azeez (رحمه الله) aliulizwa: "Yasemekana kuwa Aaisha (رضي الله عنها) alifanya Hajj na Uthmaan ibn Afaan (رضي الله عنه) bila ya mahram."

Akajibu: "Hili lahitaji ushahidi. Haifai kusema hivyo kuwa alifanya Hajj bila ya mahram bila kuleta ushahidi, lazima alikuwa na mahram. Alikuwa na vijana wa ndugu zake na ndugu yake Abdulrahmaan (رضي الله عنه), alikuwa na vijana wa dada yake Asmaa' (رضي الله عنها), na yule asemae hakuwa na mahram ni mrongo ila akiwa na ushahudi. Zaidi, hata ikiwa twakubali hivyo kuwa alifanya Hajj bila ya mahram, basi yeye si maasum (asiyefanya makosa) na Maswahaba vile vile si ma'sum. Lililo la ushahidi ni lililotajwa na Allah (سبحانه وتعالى) na Mtume (صلى الله عليه وسلم). Maoni ya fulani na fulani si ushahidi. Kendacho kinyume na Sunnah si ushahidi. Ushahidi wapatikana kwenye Sunnah Swaheeh. Hili ndilo lililo maarufu kwa wanavyuoni, na ndilo lilo na Ijmaa.

Ash-Shaafi'ee (رحمه الله) alisema: kuwa watu wote wameafikiana yakuwa ikidhihiri Sunnah ya Mtume (صلى الله عليه

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

وسلم) kwa mtu, hawi na ruhusa ya kuandama maoni ya yoyote."
Maalik (رحمه الله) alisema: "Maoni ya yeyote katika sisi yaweza kukubaliwa au kukataliwa ila mkaazi wa kaburi hili (akimaanisha Mtume (صلى الله عليه وسلم)."
Lililomaanishwa ni kuwa Waislamu na waumini waikubali Sunnah, na isipuuzwe kwa maoni ya huyu au yule, Zaidi, Aaisha (رضي الله عنها) asidhaniwe kuwa yuenda kinyume cha Sunnah, ikijulikana vyema kuwa Yeye ni faqeeha na mwenye ilmu kuliko wanawake wa ulimwengu wote, na yeye ndie aliyeisikia hadeeth kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) (fataawa al-shaykh ibn Baaz-25/361,362)
Shykh ibn Uthaymeen (رحمه الله) alisema: "ikiwa mtu atasema hadeeth hii haisemi kuwa palikuwa na mahram nao, yawezwa ikasemwa kuwa hali ya wakeze Mtume (صلى الله عليه وسلم) ilikuwa ni tofauti kwa sababu walikuwa ni Ummu al-Muumineen, si kwa sababu yakuwa mahram bali kama alama ya heshima kwao? Au yazekana kusemwa kuwa hakuna lilotajwa hapa kuhusu mahram, lakini aliwatuma Maswahaba wawili watukufu pamoja na mahram? La kwanza lawezekana na la pili pia.
Ikiwa tutakubali kaida ya kilichofichika kieleweke kwa kilicho na ufafanuzi kilicho wazi twaweza kusema nini?
Jibu ni kuwa tukubali hali ya pili, na tuseme ni lazima palikuwa na mahram pamoja nao, lakini Maswahaba wawili hawa watukufu (رضي الله عنهما) walitumwa pamoja nao kama alama ya kuwatukuza na kuwapa heshima Ummul-Muumineen (رضي الله عنها).(*Sharh kitaab al-Hajj min swaheeh al-Bukhari* (kanda ya tepu No.19 upande wa 2). Allaah (سبحانه وتعالى) ndiye Mjuzi wa Yote.

Mwanamke kwenda Hajj pamoja na kundi la Wanawake lisilokuwa na Mahram

Na: Sheikh al-Munajjid

Ameuliza mwanamke: "Mimi naishi katika nchi ya Saudia kwa sababu nafanya kazi hapo. Mwaka jana nilikwenda Hajj, na pamoja na mimi palikuwepo wanawake wawili rafiki zangu, lakini hapakuwepo na mahram pamoja na sisi. Ni nini hukmu kuhusiana na jambo hilo?"
Jawabu: "Alhamdulillaah, Amesema Sheikh Muhammad Ibn Uthaymeen (رحمه الله): 'Kitendo hiki – Hajj bila ya Mahram – ni haraam kwa sababu ya hadeeth ya Ibn Abbaas (رضي الله عنه) aliyesema: 'Nilimsikiya Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema pindin alipokuwa akitoa khutbah, 'Mwanamke haruhusiwi kusafiri isipokuwa awe na Mahram.' Akasimama mtu mmoja akasema, 'Yaa Rasoolullaah, mke wangu amekwenda Hajj, na mimi nimejisajili kwenye kundi la kwenda kupigana Jihaad.' Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia: 'Nenda ukahijji na mkeo.'" Imepokewa na al-Bukhaari, 3006; Muslim, 1341.
Kwahivyo, hairuhusiwi kwa mwanamke kusafiri bila ya kuwa na Mahram.
Mahram ni mtu ambaye kwake yeye (mwanamke) ameharamishwa milele kumuowa kutokana na mafungamano ya kidamu naye au kwa sababu inayokubalika. Jambo hili vilevile litategemea sharuti yakwamba na awe ni mwanamume aliyepita umri wa kubaleghe na mwenye akili timamu. Motto mdogo wala mtu asiyekuwa na akili timamu hawawezi kuwa ni Mahram.
Sababu ya kuwepo mahram miongoni mwa sharuti ni kwa sababu awe ni mwenye kumuhudumikia na kumlinda, ili asisumbuliwe na watu wasiomcha Allaah na wasiokuwa na rehma na waja wa Allaah.
Hapana tafauti yoyote iwapo atakuwa na kundi la wanawake wengine au laa, au emma yuko salama au laa. Hata kama atakwenda pamoja na wanawake wa kutoka kwenye familia yake akawa na usalama wa kutosha, hairuhusiwi kwake kusafiri bila ya mahram, kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipomuamrisha Yule mtu ende akafanye Hajj pamoja na mkewe, hakumuuliza iwapo alikuwa pamoja na wanawake wengine au laa, au iwapo alikuwa kwenye usalama au laa. Ukweli wa kwamba kwa vile hakumuuliza kuhusu suala hilo inaashiriya kuwa haikuleta tafauti yoyote. Huu ndio msimamo wa sawa
Baadhi ya watu siku hizi hulichukulia jambo hili kwa wepesi na kuwaruhusu wanawake wasafiri peke yao kwa Ndege bila ya mahram. Jambo hili , bila ya shaka yoyote, linakwenda kinyume na maana iliyo wazi ya maandiko. Usafiri kwa ndege ni kama usafiri mwengine wowote na vilevile unahusisha hatari. Ikiwa mahram wa mwanamke mwenye kusafiri kwa ndege atamchukuwa mpaka kwenye uwanja wa ndege, pindi atakapowasili kwenye ukumbi wa kuondokea, itambidi amuache hapo, kasha kutokea hapo atakuwa bila ya mahram. Ndege huwenda ikaondoka kwa wakati wake au huwenda ikachelewa. Inaweza kuondoka kwa wakati wake, lakini mara inaweza kurudi tena kutokana na sababu zozote ziwazo, au huwenda ikatua kwenye uwanja mwengine ambao sio uwanja alioukusudia kwenda, na mfano kama hivyo. Huwenda ikatua kwenye uwanja ulioukusudia baada ya wakati uliotarajiwa kutokana na sababu zozote ziwazo. Ikitokea yakwamba imewasili kwa wakati uliopangwa, mahram aliyekusudiwa kukutana naye huwenda akachelewa kutokana na sababu zozote ziwazo, emma huwenda ikawa alichukuliwa na usingizi au kutokana na msongamano wa magari, au kwa sababu gari lake liliharibika, au kutokana na sababu nyengine. Na hata kama atakuwa amewasili hapo kwa wakati uliopangwa nan akakutana na mwanamke, panawezekana kuwepo mtu atakaekaa kando yake ndani ya ndege awezae kumuhadaa na akampenda yeye nae akampenda (huyo mwanamke).
Nukta muhimu ni kwamba wanawake na wamche Allaah na wasisafiri kwenda Hajj au kwa sababu zozote isipokuwa wawe na mahram mtu mkubwa mwenye akili timamu. Na Allaah ndiye ambaye Msaada wake twauhitaji.
Daleel al-Akhta' allati yaqa'a fiha al-Haaj wa'l-Mu'tamir (makosa yanayofanywa na Mahujaji wenye kufanya Hajj na 'Umrah)

MFUNGWA KUKUSURU [KUFUPISHA] SWALA

Na: Shaykh Mashhor Hassan Al-Salmaan

Suala kutoka kwa ndugu wa Tunisia walioulizia: Mara nyengine mtu katika nchi yetu hufungwa na mahali anapofungwa ni mbali na mahali anapoishi na ni masafa ambayo kufupisha swala yaruhusiwa. Kwa mfano, masafa baina ya nyunba ya mtu na jela ni kama 200 km (125 ml) ikiwa yafahamika kuwa mfungwa hajui atakaa mda gani ndani ya jela wanapomkamata mwanzo humueka rumande huku akingojea hukmu. Na hukmu ya nchi huchukua muda mrefu mtu kuhukumiwa mpaka mwaka baina yakushikwa kwake na siku ya kwanza ya kusikizwa kesi. Kwahivyo suala langu ni – kutokana na uzito huu je aruhusiwa kufupisha swala wakati wakifungo chake na ni kwa muda gani ikiwa aruhusiwa ataendelea kufupisha swala?
Jawabu kutoka kwa shaykh mashhoor

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

(حفظه الله): “Hukumu na taratibu kuhusu mfungwa kwenye sharia ya dini yameelezwa kwa upana na wa kwanza katika wale walioeleza na kuonyesha hamu kubwa kuhusu mas’ala ya haki za wafungwa na taratibu za fiqh walikuwa ni wanazuoni wa ki-Hanafi wa mwanzo. Na wa mwanzo kuhusu hili alikuwa ni Abu Yusuf, mwanafunzi wa Abu Haneefah katika kitabu chake al-Kharaj na vilevile mwanafunzi wa pili wa Abee Haneefah ambaye ana daraja kubwa katika madhambi ya Hanafee ni Muhammad bin Hasan ash-Shaybaani, wote wawili wajulikana kama “Shaykhaan” katika madh-hab ya Abee Haneefah. Ash-Shaybaani ana kitabu kinachoitwa as-Siyar na kwenye kitabu hicho haki za mfungwa zimetajwa. Jumuiya ya haki za wafungwa Geneva Switzerland iitwayo Organization of Detainee Rights iliandika kitabu kiitwacho Muhammad bin Hasan ash-Shaybani chakulinda haki za wafungwa na raisi wa Organization alinizuru mimi na akasema: “Sisi tunafahari ya mtu kama huyu (Muhammad bin Hasan ash-Shaybanee) ambaye baada ya miaka mia baada ya hijra peke yake amezungumza kuhusu haki za wafungwa na waliozuiliwa (detainees) *maneno ya mfasiri – Rasheed Gonzales (حفظه الله): “Wasiokuwa Waislamu wengi katika wasomi wao na watu wa utafiti vilevile wamemtunuku Imaam Muhammad bin Hasan as-Shaybaani kwa juhudi yake kuhusu jambo hili. Rudolf Peters (e.d) katika ‘Jihad in classical and mordern Islam’: A reader (princeton, New Jersey: Mercus Weiner Publishers,1996). Uk.3-5 alisema: “Wakati wa nusu ya karne ya nane maelezo ya kwanza kwa ufafanuzi na maandishi kuhusu sheria za Jihad ziliandikwa na al-Awzai na Muhammad Shaybani.” Peters vilevile alikiri kuwa: kuwakinga wale ambao hawapigani, njia za halali za kivita, namna ya kuwaangalia mateka [na] adabu ya usawa kwa watu maadui” ni mas’ala yaliyobainishwa katika vitabu vya sharia za milango ya jihad. Peters vilevile ametaja (Uk.137) kuwa as-Siyar kimezangatia sharia za Kiislamu zinahusu maadili na wasiokuwa Waislamu.” Na hili pia limeashiriwa na Charles Cinch katika makala yake ya 2005 kuhusu jihad: Vipi yaweza kuokoa maandishi ya kidini katika vita vya uaadilifu [an analysis of just war doctrine in UCLA international institute: John strawson aliandika makala ya utafiti wake ulio maaruf 1993 kudirikana na sharia ya Kiislamu (encountering Islamic law) kuwa as-Siyar cha ash-Shaybaani “kina ndani yake sharia na hukmu za kivita... vigawanyo vyake vya sharia za kivita ambayo hakitaonekana kitu kigeni kwa mwanafunzi wa kimataifa wa kileo. Kazi yake Imaam ash-Shaybaani amemulikwa vivile na Recep Senturk (2005) katika “Socialogy of Rights” “AM THEREFORE I HAVE RIGHTS” “HUMAN RIGHTS IN ISLAM BETWEEN UNIVERSALISTIC AND COMMUNALISTIC PERSPECTIVES” ‘In the Muslim world journal of human rights’ Katika yale yaliotajwa ndani ya utafiti katika vitabu vya wanazuoni na ambapo tafauti ya maoni ipo kama kawaida, ni tafauti ikiwa: Mfungwa afupisha swala yake akiwa amefungwa au la? Yaliyotajwa katika vitabu vya wanazuoni ni wakati mfungwa akitwaliwa kutoka nyumbani kwake kupelekwa jela na jela iko mbali na nyumba yake basi afaa kufupisha swala zake akiwa njiani kuelekea jela. Kwa hivyo akiwa njiani kuelekea jela yeye ni msafiri kama yule ambaye ni mkaazi (ambaye husafiri na akafupisha swala zake na kuziunganisha). Sheria za Allah ziko wazi kwahivyo yeyote aondokae nyumbani kwake kwenda jela na jela iko mbali kutoka kwake, kwa masafa ambayo swala yafaa kufupishwa , basi na afupishe swala yake akielekea jela na haya ni maneno ya Imaam Ahmad (رحمه الله) na ni ufahamu wa madhhabi ya Malik. Hili ndilo ninaloliona kuwa la sawa kinyume na madhhabi ya ki-Shaafiiyyah , kwani Imaam ash-Shaafiee (رحمه الله) alikuwa akisema kuwa mfungwa hafai kufupisha swala zake, kwa kuwa hana nia ya kusafiri. Kwa hivyo Imaam ash-Shaafi alikuwa akiona kuwa mfungwa hana nia ya kusafiri wala safari ya masafa hayo, bali kilicho swahihi ni yule afikiliaye masafa hayo afaa afupishe swala zake inshaaAllah. Ama kwa yule anayesafiri kwa maasi, basi katika hili hairuhusiwi kwa mtu kufupisha swala wala kuacha kufunga na kutumia mambo yanayoruhusiwa kwa msafiri kuhusu ibada zote. Hii ni kulingana na Ahlul ilm. Basi sasa mtu akishatulia katika jela na mahabusu au mshikwa akiwa katika mikono mwa maadui safari yake yafika mwisho na aregea katika hali ya mwenyeji. *neno la mfasiri [baadhi ya ndugu zetu uingereza waliofungwa waonelea kuwa ni sawa wakifupisha na kuunganisha swala zao lakini kulingana na maneno ya Sh.Mash-hur yaaonyesha kufanya hivyo ni makosa] kwa hivyo mafuqahaa wanataja mas’ala haya na yana manufaa na yana tanzu ndani ya sera ya baadhi ya Ahlil ilm, kama je mfungwa atakiwa kuswali jum’ah? Ikiwa mfungwa ni msafiri basi jumu’ah si wajib kwake, na ikiwa si msafiri basi ni wajib kwake kuiswali swala ya jum’uah . lililo swahihi kutokana na maneno ya maulamaa , na ni madhehebu ya wengi wao ni kuwa jumu’ah ni wajib kwa mfungwa ikiwa ashatulia ndani ya jela. Al -Buwaytee, mwanafunzi wa Shaafiee (رحمه الله) *Maneno ya mfasiri [Imaam al-Allaamah bwana wa mafuqahaa, Abu Ya’qub Yusuf bin Yahya al-Misree al-Buwaytee, mwanafunzi wa Imaam as-Shaafiee, alikufa akiwa kwenye nyororo akiwa amefungwa Iraaq mwaka 231 AH (angalia adh-dhahabee siyar vol.12 Uk.58) kwa sababu al-Mu’tasim alikuwa ameweka kwa ugumu itikadi ya kikafiri ya mu’tazilee juu ya wanazuoni na kuwalazimisha kuitii, Abbasid walimuweka mkiuka mipaka ya Allah Ibn Abee Layth al-Asaam kuisimamisha itikadi hiyo mbovu (yakuwa Qur’an ni kiumbe cha Allah) alipokuwa yeye ni hakimu mkuu masri mwaka 226 AH/ 846 CE. Aliwanyanyasa watu wa Sunnah na akendeleza itikadi za Bid’a ; al-Buwaytee alikuwa muhasirwa wa ukafiri huo wa kuwa Qur’an kuwa imeumbwa.kila ijumaa alikuwa akijaribu kutoka jela aliposikia adhan ya jumuah akifikia milango ya jela walinzi walikuwa wakimwambia “rudi Mungu akurehemu” al-Buwaytee alikuwa akiomba duaa akisema “O Allah nimeitikia mwito wako lakini wamenizuia (kwenda kuswali Jumu’ah)” Ibn us-Subkee katika kitabu chake at-tabaqaat ash-Shaafi’iyyah al-kubraa vol,1, Uk.276 alipokea haya kutoka kwa al-Buwaytee. Linalo takiwa kuzangatiwa hapa nikuwa mfungwa nilazima asimamishe jumu’ah na maulamaa wasema ni wajibu wa walio na utawala kuwasimamishia jumu’ah wafungwa. Zamani wafungwa walikuwa wakenda nje ya jela kuswali,lakini ikiwa ijumaa yasimamishwa ndani ya jela basi ni wajibu wa kila mmoja katika waislamu wote ambao wako huru, waume, wenyeji wa jela wote watatakiwa wasimamishe swala ya jumu’ah. Ikiwa jumu’ah haikusimamishwa kwao basi watakuwa hawana madhambi kulingana na hadeeth ya Abu’l-Ja’d ad-Damaree (رضي الله عنه) kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema “Yeyote mwenye kukosa ijumaa tatu zenye kufuatana bila ya udhuru, basi Allah ameufunga moyo wake.” (at-Tirmithi, Ahmad, Ibn Majah wamepokea

(Endelea kutoka Uk. 3)

hadeethkama hii kutoka kwa Jabir ibn Abdillah) kauli yake Mtume (صلى الله عليه وسلم) “bila ya sababu...” yaweza ikawa ni udhuru kama ugonjwa, safari, kulazimishwa au kutokuwa na uwezo wa kusimamisha Jumu’ah basi hana lawama inshaAllah na pia kutoka kwa maandishi ya Imaam Sarkhasee al-Hanafee * Neno la mfasiri [Shamsuddeen Muhammad bin Ahmad as-Sarkhasee alikufa 490 AH na alitoka mji wa sarkhas au sarkhas au saraghs’ ambao ni mji uliopo leo baina ya nchi mbili katika mipaka yao. Miji hii yatafautiana katika majina yao kidogo, kaskazini mashariki ya Iran karibu na mji wa Mashhad (ambao uko karibu na Naysaboor) wajulikana kama ‘sarakhs’ na nusu nyingine yake ni Turkmenistan na wajulikana kama ‘saraghs’ au ‘saragt’ ni kuwa yeye alifungwa ndani ya kisima na kitabu chake al-mabsoot alikiandika akiwa mfungwa ndani ya kisima, Imaam as-Sarkhasee (رحمه الله) alikuwa akinukulu kitabu chake kwa wanafunzi wake waliokuwa wakikusanyika mzunguko kisimani humo (wakiangalia kweye shimo huku wakisikiza mafunzo). Imetajwa kwenye vitabu hivyo yakuwa ikiwa mfungwa anao uwezo basi asimamishe swala hiyo ya jumu’ah. Kwahivyo lilo wazi katika kumalizia mada hii nikuwa mfungwa akiwa njiani kuelekea jela yeye huwa ni msafiri na atakiwa afupishe swala yake na akitulia jela safari na hali ya safari itakuwa imefika mwisho na aregea kuwa mwenyeji na aswali jumu’ah kukiwa uwezekano na Allah (سبحانه وتعالى) ajua zaidi.

Thawabu za kuihifadhi Qur’an

Na: Sheikh al-Munajjid

Ni malipo gani atakayopata mwenye kuihifadhi Qur’an?
Alhamdulillaah.
Yoyote mwenye kuihifadhi Qur’an na akaitendea kazi, Allaah atamlipa na kumuenzi kwa utukufu kwa jambo hilo, ili amuinue daraja yake Peponi itakayofika kipimo cha kadiri alivyohifadhi Kitaab cha Allaah.
At-Tirmidhee (2914) na Abu Daawud (1464) wamepokea kutoka kwa Abdullaah Ibn ‘Amr yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: “Mwendani wa Qur’an ataambiwa: ‘Soma na upande daraja, soma kama ulivyokuwa ukisoma ulimwenguni, kwani daraja yako itakuwa kwenye aya ya mwisho uliyoisoma (ulimwenguni).”
Hadeeth hii imeorodheshwa kuwa swaheeh na Sheikh al-Albaani katika Silsilah as-Swaheehah 5/218, no. 2240, na baada ya hapo akasema:
Tanabahi yakwamba maana ya “Mwendani wa Qur’an” ni yule aliyeihifadhi kwa moyo, kama alivyosema Mtume (صلى الله عليه وسلم) “Mwenye kuijua Qur’an zaidi na awaongoze watu kwenye swala,” kwa maana yakwamba aliyehifadhi zaidi. Tafauti katika daraja Peponi zitategemea ni kiwango gani kilichohifadhiwa hapa ulimwenguni, na wala sio kiwango kitakachosomwa katika siku hiyo kama wanavyodhania baadhi ya watu. Jambo hili linaashiriya waziwazi juu ya fadhla za haafidh aliyehifadhi Qur’an, lakini hilo litategemea sharuti yakwamba ameihifadhi kwa ajili ya Allaah, na wala sio kwa ajili ya mambo ya kilimwengu au kwa ajili ya kujipatia pesa. Au kinyume chake, Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: “Wanafiki wengi wa Ummah wangu ni miongoni mwa wale waliohifadhi Qur’an.”
Ama kuhusu fadhla za hafidh aliyehifadhi Qur’an, amepokea al-Bukhaari (4937) kutoka kwa Aaisha (رضي الله عنها) yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): “Mfano wa anayesoma Qur’an na akaihifadhi ni kwamba yeye atakuwa pamoja na waandishi wema watukufu (wa Qur’an). Mfano wa mwenye kuisoma na akajaribu sana kuihifadhi hata kama itakuwa ni ngumu kwake, atakuwa na malipo sampuli mbili.”
Kwa haafidh aliyeihifadhi Qur’an, kuswali qiyaam ni rahisi kwake. Na Qur’an itmuombea katika siku ya kufufuliwa, kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: “Saumu na Qur’an zitawaombea vipenzi vyao katika siku ya Kufufuliwa. Itasema Saumu: ‘Ewe Mola, mimi nilimnyima chakula na matamaniwa yake katika wakati wa mchana, basi nakuomba unikubalie nimuombee nae.’ Na Qur’an nayo itasema: ‘Ewe Mola, mimi nilimnyima usingizi wake wakati wa usiku, basi nakuomba nimuombee nae.’ .” Imepokewa na Ahmad, al-Tabaraani na al-Haakim; ikaorodheshwa kuwa swaheeh na al-Albaani katika Swaheeh al-Jaami’, no. 3882. Na Allaah Ndiye Mjuzi zaidi.
Inataka ifahamike hapa yakwamba kuna hadeeth iliyo dhaifu inayonukuliwa kuhusiana na fadhla za kuhifadhi Qur’an. Hadeeth hii yasema, “Aliyehifadhi Qur’an, iwapo atazingatia inayohalalisha kuwa ni halali na inayokataza kuwa ni haraam, basi atawaombea watu kumi katika jamii yake katika siku ya Kufufuliwa, wote ambao waliokuwa wamehukumiwa kuingia Motoni.” Hii imepokewa na al-Baihaqee katika Shu’ab al-Imaan (vitagaa vya Imaan) kutoka kwa Jaabir. Imeorosheshwa miongoni mwa hadeeth dha’eef na Sheikh Al-Albaani katika Dha’eef al-Jaami’.

TANGAZO LA SWALA YA 'ЄID

THE QUR’AN & SUNNAH SOCIETY OF EAST AFRICA [QSSEA]

TUNAFURAHA KUWATANGAZIA SWALAAT UL ‘EID ITAKAYOSWALIWA KATIKA UWANJA WA **CONGO BOYS [MBARAKI POLICE].** ITAKUWA NI SIKU YA PILI BAADA YA MAHUJJAAJ KUSIMAMA KATIKA UWANJA WA ARAFA [9th Dhul-Hijjah, 1432] SWALA ITASWALIWA **SAA MOJA NA NUSU 7:30 AM** ASUBUHI. TWAWAOMBA MUJE NA MISWALA YENU NA WUDHU WENU INGAWA MAJI NA MIKEKA ITAKUWEPO. NAFASI ZA WANAWAKE PIA ZITAKUWEPO, NAO WAJITOKEZE KWA WINGI KAMA ILIVYO SUNNAH YA BWANA MTUME MUHAMMAD **(صلى الله عليه وسلم)**

VILEVILE KUTAKUWA NA NAFASI YA KUEGESHA MAGARI NA USALAMA UTAIMARISHWA.